

Swahili transcript:

Sherehe ya kitchen party inamwandaa huyu dada ambaye anategemewa kuwa mama ili akawe mama mwema katika familia yake. Kwa hiyo ndio maana wanamletea vyombo vya jikoni ili hata wageni wakija aweze kuwahudumia,aweze kuwakarimu wageni, kuwapikia chakula, kuwapa vinyaji, na vilevile hata akiletewa vyombo, vile vifaa vya usafi, ni kwamba wanamfundisha huyu dada ambaye anategemewa kuwa mama kuwa yeye ndiye jukumu lake la kufanya usafi, kuhakikisha aah! familia inaishi katika hali ya usafi, nyumba safi,vyombo safi,kila kitu safi na yeye mwenyewe pia. Kwa hiyo kunakuwa na nasaha mbalimbali ambazo zinatolewa kwa huyu binti ambaye anategemewa kuwa mama. Kwa hiyo wanatoa nasaha mbalimbali kwamba labda aah! unaolewa na ukifika huko jitahidi kuwapenda ndugu wa pande zote mbili, labda ndugu, wazazi wa mume, wazazi wako,ndugu wa pande zote mbili, vilevile ukawe mkarimu ndio maana tunakupa vyombo hivi, labda sufuria hizi,sahani hizi,ukapike, wageni wakija uwapikie, uwape chakula,aah! labda tunakupa mfangio huu au vyombo hivi vya usafi ili kwamba nyumba yako iwe nzuri, iwe safi wakati wote, kwa sababu mama ndiye ambaye anategemewa kuwa msafi pale nyumbani. Kwa hiyo sherehe hii ya kitchen party ni nzuri sana katika utamaduni wa kitanzania, na ni kweli imefanyika kuwa ni bora kwa sababu inawaandaa mabinti katika suala zima la kuanza familia yaani katika maisha ya ndoa. Pia kunakuwa na vitu vingi ambavyo vinaongelewa katika sherehe hii ya kitchen party, lakini mara nyingi inakuwa ni katika mausia yale ambayo yanatolewa ni katika kumweka huyu dada ili aweze kuwa mama mwema katika familia. Kwa hiyo anapewa vile baadae baada ya zile nasaha, wanakuja wakina mama wanatoa zile zawadi, wanampa zawadi, wanampongeza, wengine wanatoa pesa, wengine wanatoa chochote ambacho mtu anacho, lakini ambacho anajua kwamba kitamsaidia huyu mama ambaye anaianza familia ili aweze kufanya vizuri katika familia yake. Kwa hiyo kunakuwa na vitu mbalimbali ambavyo vinatolewa, na kama nilivyosema mwanzoni kwamba inategemea kama wazazi wa huyu binti wana uwezo au ana ndugu ambao wana uwezo, sherehe inakuwa ni kubwa sana. Anaweza akaletewa hata zawadi labda ya kabati la nguo,kabati la vyombo, au jiko

la kupikia, au jiko nikimaanisha jiko labda jiko la umeme, au anaweza akanunuliwa hata friji kwa ajili ya kuhifadhia vyakula, anaweza akanunuliwa vitu vingi vya thamani inategemea na familia ambayo yule binti anatoka. Na katika wengine ambao wanatoka katika familia ambazo uwezo wao ni wa kawaida, yaani wako katika maisha tu ya kawaida, basi anapewa vitu vingine tu ambavyo navyo ni vya msingi katika binti huyu kuanza familia yake. Mara nyingi sherehe hizi za kitchen party zimefanyika katika miji mikubwa. Na katika aah! vijijini huwa sherehe hizi huwa mara nyingi hazifanyiki. Ni katika miaka hii ya karibuni ndio sherehe hizi zimepata umaarufu mkubwa hasa katika miji mikubwa kama Dar es salaam, Arusha, Mwanza na miko mingine ambayo kidogo hali iko juu. Kwa hiyo sherehe hii ni nzuri kama nilivyosema mwanzoni kwamba inamsaidia huyu binti, kwa hiyo hata kama alikuwa labda hana uwezo sana wa kununua kila kitu, lakini kutokana na hawa wamama wanajitolea, wanatoa pesa zao, wananunua vitu, vinamsaidia huyu binti kuanza maisha yake ya ndoa akiwa na vitu vyake mle ndani kuweza kufanya vizuri hata katika ndoa. Kwa hiyo ni sherehe ambayo ni nzuri sana kwa watanzania.

English translation:

As I said, a kitchen party prepares a young lady to start her own family. When women bring her kitchen utensils, they are actually teaching her to be a generous person so that when guests visit her, she can cook for them and she can buy them drinks. As for the cleaning tools, they teach her to be smart. It is her responsibility to make sure that her family lives in a clean environment, a clean house, and she is also expected to be smart. So women prepare words of wisdom which they will pass on to this young lady (mother to be). Some of them say things like “Now you’re getting married, try your best to love the relatives of both families, go and be a generous person, that is why we give you these kitchen utensils so that when guests come, you can cook for them.” “We give you some cleaning tools so that your house will be clean all the time, because you’re expected to be a smart mother.” As I said, a kitchen party celebration is so good because of its goal of preparing young ladies on the way to starting their married lives. During a kitchen party, women advise the bride on all the things they know will help the bride-to-be in her new married life. After that, they give her presents that they have prepared for her. Some give

her money, and anything else that will help this young lady with her own family. As I pointed earlier, if her parents are rich, the celebration will also be big and she will get many precious presents like cupboards, gas stove, a fridge, et cetera. For those whose parents are not rich, they also get good, important things which will be useful as they start their married lives. Kitchen parties are mostly held in big cities, not in villages. In recent years, these celebrations gained popularity especially in big cities like Dar es Salaam, Arusha, Mwanza and other regions with high status. As I said, a kitchen party is good because it helps even those who don't have enough money to start their families off with the important things. So the women organize themselves and buy things for her. It is a good celebration for many Tanzanians.

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated